

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO



16.06.2021.

## TANGAZO LA ZABUNI ZA MAWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO NA HUDUMA YA ULINZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA KIPINDI CHA KUENZIA JULAI 2021 – JUNI, 2022.

Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro inawatangazia wale wote wanaotaka kuomba zabuni za kukusanya mapato kwa kipindi cha Julai, 2021 mpaka Juni, 2022, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 7 ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013, pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016, wanakaribishwa kuomba zabuni hizo kama ifuatavyo hapo chini.

### UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO.

#### FUNGU LA 1: UWAKALA WA KUKUSANYA USHURU WA SAMAKI .

Na.	ZABUNI	KATA	CHANZO
1.	LGA/062/2021-2022/NC/01	SHAMBARAI	USHURU WA SAMAKI BWAWA LA KIDAWASHI

#### A. MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI ZA UWAKALA WA KUKUSANYA USHURU WA SAMAKI.

Maombi yote ya Zabuni yazingatie masharti yafuatayo:

#### MASHARTI YA JUMLA

1. Kila mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania.
2. Mapato yote yatakayokusanywa na wakala yataingizwa katika akaunti ya Halmashauri na Wakala atarejeshewa asilimia ishirini (20%) na Halmashauri kama ada ya makusanyo ya kiwango kwa mwezi. Muda wa malipo kwa wakala ni ndani ya siku kumi na nne (14) ya mwezi unaofuata baada ya wakala kuleta hati ya madai ya mwezi husika. Wakala afanye utafiti na kuonyesha kiwango cha juu cha mapato atakachowasilisha Halmashauri.
3. Mwombaji awe na uwezo wa kukusanya Mapato kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (**Electronic Revenue Collection System**) na mafunzo juu ya mfumo huo yatatolewa.
  - (i) Mfumo wa kielektroniki unaotumika na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ni "**Local Government Revenue Collection Information System – LGRCIS**". Wakala atatakiwa kutumia vifaa vya kukusanya Mapato (**Point of Sale- POS**) ambavyo vitakuwa vimeunganishwa na mfumo wa ukusanyaji Mapato (**LGRCIS**) wa Halmashauri.